BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Pili – Tarehe 26 Novemba, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake.

II. MASWALI:

1. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Swali Nam.142: MHESHIMIWA SAID ALI MBAROUK (JIMBO LA GANDO) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa Muwekezaji aliyeruhusiwa kuwekeza katika pwani ya eneo la Ukutani, Shehia ya Ukunjwi, Wilaya ya Wete amefyeka na kuteketeza mikandaa (mikoko) mingi bila ya kusikiliza kilio cha wananchi.

(a) Kwa nini Serikali imemuachia Muwekezaji huyu kufanya uharibifu huo wa mazingira.

(b) Je, uwekezaji wa Muwekezaji huyo una thamani gani na una faida gani kwa wananchi wa vijiji vya Shehia ya Ukunjwi.

2. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Swali Nam. 203: MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (NAFASI ZA WANAWAKE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara

Maalum za SMZ:

Tumeona Kamanda wa Kikosi cha KMKM akiahidi kutoa huduma ya kuwavusha wananchi wanaoishi maeneo ya visiwani kama Tumbatu, Njao, Fundo na visiwa vyenginevyo.

Je, ni lini kazi hii itaanza rasmi

3. Wizara ya Uwekezaji:

Swali Nam. 130: MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (JIMBO LA OLE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji:

Zipo tetesi zinazoeleza kwamba, miongoni mwa visiwa vilivyokodishwa ni pamoja na Kisiwa cha Kwale kinachotumiwa na Wananchi wa Fumba, Bweleo, Kikungwi na Unguja Ukuu.

(a) Je, Tetesi hizo zina ukweli gani.

(b) Kama ni kweli kimekodishwa kwa muekezaji gani na kwa gharama gani.

4. Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Swali Nam.16: MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Utaratibu wa kuingiza nishati ya mafuta uliokuwepo zamani, ulikuwa wa kiushindani na kufanya upatikanaji wa nishati hiyo kuwa wa uhakika. Hata hivyo, hivi sasa utaratibu huo umekuwa wa ukiritimba kwa kuwepo muingizaji mmoja peke yake (monopoly).

(a) Kwa kiasi gani utaratibu huo wa kuwepo mletaji mmoja wa nishati haupingani na Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara.

(b) Kuna faida gani kubwa ya kuwa na mletaji mmoja peke yake wa nishati ya mafuta hapa nchini.

(c) Kuna hasara gani inayohofiwa kwa kuwa na ushindani halali katika uletaji wa nishati ya mafuta nchini.

5. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Swali Nam.68: MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (NAFASI ZA WANAWAKE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Elimu ni ufunguo wa maisha na hauwezi kupatikana bila ya kupitia kwa walimu. Hata hivyo, hivi sasa kumejitokeza mtindo wa baadhi ya wanafunzi kuwashambulia walimu ambao wanawafundisha na kuwajenga katika misingi imara.

Je, kuna mikakati gani itayotumika ya kuwalinda na kuwanusuru walimu, ili heshima yao isiendelee kushuka.

6. Wizara ya Afya:

Swali Nam.59: MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (JIMBO LA ZIWANI): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Kituo cha Hospitali ya Gombani kimekuwa tegemeo kwa wakaazi wa majimbo yote yaliyolizunguka kituo hicho hususani kwa utoaji wa huduma ya Mama na Mtoto. Na kwa kuwa eneo la utoaji huduma hizo ni dogo ambapo hupelekea wagonjwa kusambaa hadi kwenye ukingo wa Barabara, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wao.

(a) Je, ni lini Serikali imefuatilia na kubaini tatizo hilo.

(b) Je, lini Serikali itachukua juhudi za dharura za kujenga kituo cha kisasa katika eneo hilo kabla ya maafa kutokea.

Swali Nam.96: MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (JIMBO LA OLE): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna malalamiko kwamba baadhi ya wategemezi muhimu wa mwanachama wa Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF), hususani Mwenza na Wazazi/Wazee, hawapati huduma kupitia uanachama wake bila ya kulipiwa gharama za ziada.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Mfuko wa Huduma ya Afya ya Zanzibar, ili kuongeza wigo wa wategemezi wa mwanachama, hususani Mwenza na Wazazi/Wazee.

(b) Je, ni sababu gani zinazofanya makundi hayo

kutonufaika moja kwa moja kupitia uanachama wa mtegemezi wao bila malipo ya ziada.

(c) Je, Serikali imefanya tathmini ya gharama na uwezekano wa kuwajumuisha wategemezi hao katika vifurushi vya bima.

Swali Nam.176: MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (JIMBO LA WETE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wananchi wa Wete, hufuata matibabu ya afya zao katika Hospitali ya Kinyasini, huku wakipata usumbufu mkubwa na hasa ikizingatiwa kuwa barabara ya kufika hospitalini hapo haina daladala za uhakika, hali inayowalazimu kutegemea usafiri wa bajaji, ambao wengi wao hawauwezi kutokana na kupanda kwa nauli.

Kwa nini Serikali haioni umuhimu wa haraka wa kuifungua Hospitali ya Jadida, ili kupunguza shida kwa Wananchi wa Wete.

7. Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Swali Nam. 131: MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (JIMBO LA OLE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imefanya uwekezaji mkubwa wa kujenga eneo la maonesho na Kituo cha Mikutano, katika eneo la Nyamanzi.

Je, uwekezaji huo wa Serikali umetumia kiasi gani.

8. Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Swali Nam. 198: MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (JIMBO LA WETE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Mabadiliko ya vipindi katika Redio Zanzibar (ZBC Radio), yameendelea kugusa hisia za wasikilizaji wengi, hasa wasikilizaji wazuri wa kuvisikiliza vipindi hivyo, ikiwa ni pamoja na kipindi cha Kutoka Vijijini, Wajibu Kazini na Uguwa Pole.

(a) Je, ni sababu gani iliyopelekea vipindi hivyo kuondolewa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vipindi hivyo vinarejeshwa na kuendelea kusikilizwa.

9. <u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>

Swali Nam. 71: **MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (NAFASI ZA WANAWAKE) -** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kuna sababu gani zilizopelekea wakati wa ku-*renew* leseni kuwe na mafunzo ya madereva ambao wanatafuta huduma hii, wakati mafunzo hayo yangelitolewa tu kwa madereva wanaotaka kupewa leseni kwa mara ya kwanza.

Swali Nam. 110: **MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (JIMBO LA WETE) -** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Taasisi zetu za ndani hasa za Usafiri wa Baharini zinawabana sana Mabaharia kwenye maslahi na hata muda mwengine huwatishia kuwafukuza kazi, jambo ambalo ni kero na adha kubwa hasa kwa Mabaharia wa Kike.

(a) Ni lini Serikali itatunga Kanuni nzuri zitakazowaongoza na zisizowabana Mabaharia hao, ili ziweze kuwasaidia wakiwa kwenye majukumu yao ya kazi za kila siku.

(b) Kwa kuwa mikataba ni haki ya Mabaharia, je, Serikali lini itatoa angalau muongozo wowote kwa taasisi hizo, ili kuheshimu na kufuata utaratibu.

Swali Nam. 117: **MHESHIMIWA MOZA MOHAMMED KHAMIS (NAFASI ZA WANAWAKE) -** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na uchukuzi:

Kwa kuwa Bandari zetu za Zanzibar zina Wabeba Mizigo wanaojuulikana kama Wachukuzi (*Potters*) ambao wanatakiwa walipe kiasi fulani ili wapatiwe beji. Na kwa kuwa hutakiwa kulipia shilingi 500 kwa kila mzigo wanaoubeba, pesa ambayo inalipwa kawaida tu, bila ya risiti

yoyote.

(a) Kwanini pesa hizi zinalipwa bila ya kutolewa risiti.

(b) Ni shilingi ngapi Mchukuzi (*Potter*) anatakiwa kulipa kwa mujibu wa sheria.

10. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

Swali Nam. 24: MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (JIMBO LA PAJE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na malalamiko kwa vijana wa Jimbo la Paje waliojiajiri katika sekta ya utalii, hasa wanaokodisha vyombo vya usafiri kwa watalii, wakilalamikia kuongezwa ada ya vibali (*permit*) kwa wageni wanaokwenda maeneo ya vivutio ambayo imefikia shilingi 50,000/, wakati wao wanakodisha vyombo hivyo kwa bei ya chini shilingi 30,000/. Ongezeko hilo limepekelea wageni kupunguza kukodi vyombo hivyo na kuwakosesha riziki vijana waliojiajiri wa Jimbo la Paje.

(a) Je, Wizara yako ipo tayari vipi kukaa pamoja na vijana hao, ili kuwasikiliza kilio chao na kutafuta njia ya kunusuru ajira zao kutokana na ongezeko la ada ya vibali kwa wageni.

(b) Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutaka kuongeza mapato yake, je kuna mpango gani utakaofanyika wa kuhakikisha kuwa, hatua itakazozichukua za kuongeza mapato, hazileti athati kwa ajira za vijana wa Paje.

(c) Kwakuwa malalamiko ya vijana hao yamekuwa ya muda mrefu sasa, je kuna hatua gani zilizochukuliwa kuwayashughulikia malalamiko hayo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na Kutunga Sheria ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuhakikisha usalama, afya na ustawi wa watu kazini na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari zinazotokana na shughuli za kazi na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
26 Novemba, 2026.

(Hassan A. Haji)
KATIBU,
BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR.